TANGAZO LA SERIKALI NA.190 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MAYA MAYA 'B' YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Maya Maya 'B' ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji)kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA1 yenye majira - nukta 810246.010MS, 9362474.945KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ100$^0$23''MS kwa umbali wa kilomita 0.48 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA2 yenye majira - nukta 810723.270MS

,9362387.414KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini– Magharibi kwa kukatisha barabara ya Dodoma - Arusha katika uelekeo wa KS85$^{0}$27’’kwa umbali wa kilomita 0.52 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA3 yenye majira - nukta 811250.878MS, 9362427.352KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ100$^{0}$23’’MSkwa umbali wa kilomita 0.36 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA4 yenye majira - nukta 811618.996MS, 9361987.469KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS164$^{0}$’MG kwa umbali wa kilomita 0.86 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA5 yenye majira - nukta 811392.MS, 9361155.685KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS162$^{0}$23’’ kwa umbali wa kilomita 0.71 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA6 yenye majira - nukta 811371.572MS, 9360443.876KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS163$^{0}$52’’MS kwa umbali wa kilomita 1.00 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MA7 yenye majira - nukta 811624.127MS, 9359468.579KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS130$^{0}$37’’MG kwa umbali wa Kilomita 0.43 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA8 yenye majira - nukta 811377.894MS, 939359115.222KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KZ144$^{0}$54’’MG kwa umbali wa kilomita 1.07 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya MA9 yenye majira - nukta 810371.429MS, 9358746.710KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini -Magharibi kwa kukatisha barabara ya Dodoma - Arusha katika uelekeo wa KS145$^{0}$’05’’MG kwa umbali wa kilomita 0.36 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA10 yenye majira - nukta 810018.458MS, 9358835.387KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ103$^{0}$57’’kwa umbali wa kilomita 0.95 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA11 yenye majira - nukta 810021.980MS, 9359780.138KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG159$^{0}$23’’ kwa umbali wa kilomita 0.75 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA12 yenye majira - nukta 809760.145MS, 9360485.453KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS153$^{0}$16’’MG kwa umbali wa kilomita 1.48 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA13 yenye majira - nukta 809925.130MS, 9361959.723KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi kwa kukatisha barabara ya Babayu - Dodoma katika uelekeo wa KZ154$^{0}$29’’MG kwa umbali wa kilomita 0.60 hadi ulipoanzia.”

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*